

# NIPASHE UK 3 Radi yaua ng'ombe zikitoka malishoni

**Na Neema Hussein, KATAVI**

NG'OMBE 28 za wafugaji watano katika kijiji cha Kabage wilayani Tanganyika mkoani Katavi zimepigwa radi wakati zikitoka malishoni.

Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Maico Kushoka, alisema tukio hilo lilitokea Jumatmosi jioni baada ya mvua kunyesha ikiambatana na radi.

Alisema wachungaji hao walikuwa na ng'ombe 42 kati yao 28 zilipigwa radi wakati wakirudi nyumbani kutoka machungani mvua ilipoanza kunyesha.

"Waliona mwanga wa radi wakatawanyika baadaye waliona ng'ombe mmoja amekufa, wakaenda kutoa taarifa nyumbani," alisema Kushoka.

Alisema baada ya kurudi waliona zingine 27 zimekufa, ng'ombe tisa zilikuwa mali ya Sitta Busheneli, Mwanamazuri ng'ombe 8, Masanja 5, Makune 4 na wawili hazikutambulika mmliki.

Aidha, alisema kiongozi wa kimila alifika eneo hilo kufanya tambiko la kimila kisha wananchi walichinja na kugawana kitoweo.

Alisema tukio hilo ni la pili kutokea mwaka 2018 zilikufa ng'ombe nne kwa kupigwa radi, lakini tukio la jana nyumba tatu zilibomoka na barabara imekatika, lakini hakukuwa na madhara kwa binadamu.

Sitta Busheneli ambaye ng'ombe zake 9 zilipigwa radi, alisema alipokea taarifa hizo kwa masikitiko makubwa na kwamba kitendo hicho kimemrudisha nyuma kimaendeleo.